DIGNITY FOR ALL
LGBTI ASSISTANCE PROGRAM

Dignity for All: Mpango wa Usaidizi wa LGBTI unatoa fedha za dharura, ufadhili wa utetezi, na usaidizi wa usalama kwa watetezi wa haki za binadamu na mashirika ya jamii yaliyo katika hatari ya vitisho au mashambulio kutokana na kazi yao ya haki za binadamu kwa LGBTI. Karatasi ya ukweli inayofuata inafafanua anayestahili na jinsi ya kutuma ombi la ufadhili.

## DIGNITY FOR ALL NI NINI?

Dignity for All inatoa usaidizi wa dharura wa kifedha kwa watetezi wa haki za binadamu na mashirika ya jamii yaliyo hatarini ili yaweze kuendelea na kazi yao. Dignity for All pia hufadhili kampeni za utetezi zilizolengwa na za wakati maalum ili kukabiliana na vitisho au mashambulio kwenye haki za binadamu kwa LGBTI na kazi ya haki za binadamu, na pia usaidizi kwa waathiriwa au jamii zinazohusiana na kampeni za utetezi zilizofadhiliwa. Mafunzo ya usalama yanapatikana ili kusaidia mashirika kuendelea na kazi yao kwa usalama zaidi.

## NI NANI ANAYESTAHILI?

Watetezi wa haki za binadamu au mashirika ya jamii yanastahili kwa ufadhili ikiwa yameshambuliwa kwa sababu ya kazi yao ya haki za binadamu kwa LGBTI. Mtetezi wa haki za binadamu (HRD) ni mtu ambaye anafanya kazi kwa amani ili kudumisha na kulinda haki za binadamu na uhuru msingi. Shirikla la jamii (CSO) linafafanuliwa kama kikundi kilichoundwa cha wanaharakati wawili au zaidi wanaofanya kazi pamoja kuhusu haki za binadamu. CSO haihitaji iwe imesajiliwa rasmi ndipo iweze kufadhiliwa na Dignity for All, lakini lazima iweze kuweka kumbukumbu ya miezi sita ya uanaharakati. Katika hali fulani, kuhusiana na kampeni za utetezi, Dignity inaweza kufadhili wanajamii binafsi.

## FEDHA ZA UFADHILI ZINATOKA WAPI?

Dignity for All hupokea michango kupitia hazina ya ufadhili ya kimataifa ya serikali na wakfu mbalimbali wa kujitegemea inayofadhili haki za binadamu kwa LGBTI.

## DIGNITY CONSORTIUM NI NINI?

Dignity for All inaendeshwa na Consortium ya mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu, ikiwemo: Akahatá, Equipo de Trabajo en Sexualidades y Géneros; the European Region of the International Lesbian, Gay, Bisexual, Trans, and Intersex Association (ILGA-Europe); Freedom House; Synergia - Initiative for Human Rights; OutRight Action International; na UHAI – Mradi wa Afya ya Ngono na haki wa Afrika Mashariki.

## FEDHA ZA DHARURA

Dharura ni nini? Dharura ni haja ya haraka ya usaidizi unaotokana na vitisho kwa HRD au CSO kwa ajili ya kazi yao. Mambo yanayopaswa kuzingatiwa yanajumuisha: wakati dharura ilipotokea na ikiwa HRD au CSO inakabiliwa na shtaka au kesi nyingine za kisheria, hatari za usalama, kupoteza mali au vifaa, au jeraha au kufungwa.

Ni aina zipi za ufadhili wa dharura zinatolewa? Dignity for All itawapa HRD na CSO ruzuku ndogo na za muda mfupi za dharura kwa ajili ya gharama za matibabu, uwakilishi wa kisheria, ziara za gerezani, ufuatiliaji wa kesi, uhamaji wa muda, ufadhili wa kutegemea, usalama, kubadilisha vifaa na aina nyingine za gharama za dharura. Kulingana na ufafanuzi, usaidizi wa dharura una mpaka na hutolewa ili kushughulikia tishio nyeti kwa wakati. Dharura pia inaweza kujumuisha haja ya zaidi ya aina moja ya usaidizi (yaani matibabau na kisheria, ubadilishaji wa vifaa).

**Dignity for All: Mpango wa Usaidizi wa LGBTI**
info@dignitylgbti.org

## NI VIPI UNAVYOWEZA KUWASILISHA OMBI KWA AJILI YA UFADHILI WA DHARURA?

Maombi yanaweza kuwasilishwa na CSO au HRD moja kwa moja au kurejelewa kwa niaba ya HRD au CSO. Tafadhali toa maelezo mengi ya kina iwezekanavyo kuhusu ni kwa nini msaada wa dharura unahitajika. Dignity hupokea maombi kupitia barua pepe kwa info@dignitylgbti.org. Timu ya Dignity inaweza kutoa usaidizi fulani wa kutumia mbinu salama za mawasiliano.

Ni vipi tunavyoshughulikia maombi ya dharura? Tunakagua maombi yote ili kutambua ikiwa yanatimiza vigezo vya ustahili (vilivyolezwa hapo juu) na ikiwa fedha zilizoombwa ni halali. Utaratibu wa kukagua unathibitisha kwa uhuru maelezo yaliyotolewa na aliyetuma ombi.

## UFADHILI WA UTETEZI

Ni aina zipi za ufadhili wa utetezi zinatolewa? Dignity itafadhili CSO kwa miradi midogo na ya muda mfupi ya utetezi ili kupambana na vitisho vya haraka kama vile sheria iliyopendekezwa au iliyopitishwa hivi majuzi, msako wa ghafla wa serikali, ongezeko la viwango vya dhuluma au hatari/tabia nyingine za dharura au kutumia vizuri fursa za utetezi za wakati maalum.

Ni vipi unavyoomba ufadhili wa utetezi? Wasiliana na shirika lanachama la Dignity Consortium kwa pendekezo la shughuli ya dharura ya utetezi ya muda mfupi iliyokusudiwa kuwa na matokeo makubwa kwenye haki za binadamu kwa LGBTi. Maombi yanapaswa kutoa maelezo mahususi kuhusu suala ambalo shughuli iliyopangwa itaangazia, eneo na muda, na bajeti yenye maelezo ya kina. Dignity for All haiwezi kutoa ufadhili wa pango wa muda mrefu.

## MAFUNZO YA USALAMA

Ni aina gani ya mafunzo ya usalama yanatolewa? Dignity Consortium hutoa warsha na mafunzo ya usalama wa kujilinda ili kusaidia LGBTI, CSO, jamii na HRD kuunda mipango ya usalama. Ufadhili huu unakusudiwa kuboresha usalama wa wanaharakati na mashirika ya LGBTI na kusaidia kuzuia vitisho na mashambulio ya siku za usoni kuvuruga kazi ya haki za binadamu kwa LGBTI

Ni vipi unavyoomba ufadhili wa usalama? Wasiliana na shirika lanachama la Dignity Consortium kwa ombi kwa ajili ya usaidizi wa usalama, maelezo ya aina ya mafunzo ya usalama yanayohitajika, na vitisho vyovyote vya sasa. Mafunzo yanaweza kufanywa kwenye eneo au kutolewa kwa mbali kupitia simu, Skype, au njia nyinginezo.

## WASHIRIKA WA DIGNITY CONSORTIUM


**Akahatá:**
Fernando D’Elio, fdelio@akahataorg.org

**Freedom House:**
Urooj Arshad, arshad@freedomhouse.org

**UHAI:**
Mukami Marete, mukami@uhai-eashri.org
Stellah Bosire, stellah@uhai-eashri.org

**Synergia - Initiative for Human Rights:**
Matthew French, contact@synergiaihr.org

**ILGA-Europe:**
dignity@ilga-europe.org

**OutRight Action International:**
Maria Sjödin, hello@outrightinternational.org